# Makubaliano ya Ridhaa Huru ya Uelewa
# Baina ya
# Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)
# Na
# Jamii ya Watataru wa Mwamayoka

## Utangulizi

Yafuatayo ni Makubaliano ya Ridhaa Huru Ya Uelewa (Makubaliano ya FPIC) baina ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na Jamii ya Wa-Taturu wa Mwamayoka, Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora nchini Tanzania kunakili makubaliano ya EACOP kuheshimu maombi ya Jamii kwamba makaburi (yajulikanayo kama Bung'eda kwa lugha yao) ambayo yana umuhimu wa pekee ki-utamaduni na ki-ibada yasihamishwe kupisha ujenzi wa bomba la mafuta. EACOP imeridhia kupindisha bomba la mafuta ili kuepusha madhara (yatokanayo na) uhamishwaji wa Bung'eda na kuheshimu haki ya wanajamii kuwa na Ridhaa Huru ya Uelewa (FPIC) kuhusu maeneo yenye umuhimu ya kipekee wa urithi kwa mujibu wa Kipengele cha 7 cha IFC kinacho husu jamii za pembezoni.

Makubaliano haya ya FPIC pia yana dhihirisha dhamira pana ya EACOP kushirikisha na kutatua madhara kwa Jamii za Pembezoni zinazojitambua kama watu wa asili ambao wana pitiwa na mradi, kwa namna inayo endana na mila na desturi zao, na kuheshimu vigezo vya kitaifa na kimataifa vya haki za binadamu. Inatekeleza dhamira iliyowekwa na EACOP na viongozi wa kimila wa Jamii ya Watataru katika Mpango Makakati wa EACOP kwa Jamii za Pembezoni zinazo jitambua kama Watu wa Asili (Mpango wa EACOP) unao fafanuliwa hapa chini. Pia ni kudhihirisha utayari wa jamii na ridhaa yao kuhusu shughuli za EACOP katika jamii zao, sambamba na dhamira iliyo fafanuliwa katika Mpango wa EACOP.

## Dhamira ya EACOP

Dhamira ya EACOP kwa Jamii ya Wataturu (Pamoja na Jamii zingine za Pembezoni wanaojitambua kama watu wa Asili) yamenakiliwa katika Mpango wa EACOP, ambao uli sainiwa na viongozi wa Kimila wa Wa-Taturu, Wa-Barbaig, Wa-Akie na Wa-Maasai Arusha, Tanzania 16 Septemba 2022.[1] Dhamira hiyo ina jumuisha:

(a) Kuwezesha ushirikishwaji wenye tija;
(b) Kujengeana uwezo;
(c) Kuwezesha uwepo wa utatuzi wa migogoro unao endana na mila na desturi;
(d) kushughulikia madhara yanayoweza kutokea kutokana na kazi za mradi wa EACOP
(e) Kuendeleza manufaa ya kiuchumi; na

[1] Maandalizi ya Mpango wa EACOP ulitanguliwa na kusainiwa kwa Dira ya EACOP ya Jamii za Pembezoni zinazojitambua kama Watu wa Asili (Dira ya EACOP), iliyo sainiwa na EACOP na viongozi wa mila wa Wa-Taturu, Wa-Barbaig, Wa-Akie na Wa-Maasai Arusha Tarehe 28 Mwezi wa Kumi 2021.

(f) Kuwasiliana na Serikali kama itakavyohitajika.

Hususan, Mpango wa EACOP una jumuisha ahadi ya "kutathmini na kupendekeza namna ya kupisha maeneo ya ibada popote itakapowezekana kiufundi"- Tazama Sehemu ya 4(d). Utekelezaji wa dhamira katika mpango wa EACOP kwa jamii ya Wa-Taturu wa Mwamayoka pia imefafanuliwa katika Wasifu wa Jamii ya Mwamayoka ambayo imeambatanishwa katika Mpango wa EACOP.

## Ridhaa ya Jamii Kuhusiana na Shughuli za Mradi wa EACOP.

Jamii ya Wa-Taturu wa Mwamayoka wanaridhia shughuli za Mradi wa EACOP katika maeneo yao wakati wa maandalizi, ujenzi na mwendelezo wa shughuli za mradi wa bomba. Kupitia mpango unao endelea wa ushirikishwaji wenye tija baina ya Jamii ya Wataturu na viongozi wa kimila, EACOP inashughulikia madhara yanayoweza kujitokeza yanayohusiana na shuguli za mradi-ikiwa ni Pamoja na kukwepa madhara kwenye Bung'eda-na itaendeleza manufaa ya kiuchumi kwa namna inayo endana na mila na desturi. EACOP ita wezesha ujenzi wa uwezo kusaidia jamii ya Wa-Taturu kuelewa na kushiriki katika shughuli za mradi kwa namna inayo endana na mila na desturi. EACOP pia itawezesha kuwepo kwa namna ya utatuzi wa migogoro na kuwezesha mawasiliano ya Wa-Taturu na Serikali.

## Kukwepesha Bomba La Mafuta ili Kuondoa Madhara katika Bung'eda

Kwa kuzingatia kwamba jamii ya Wa-taturu ni jamii ya pembezoni, na Kwa kuzingatia Madhara ya EACOP yanayo weza kutokea kwenye eneo lenye umuhimu wa kipekee ki-mila na ki-ibada, ushirikishwaji wa ziada ulifanyika kwa kujumuisha wana jamii wote Pamoja na viongozi wao wa kimila, hivyo kuwezesha kuwepo kwa Makubaliano haya ya FPIC.

Wakati wa Ushirikishwaji huo wa ziada, Jamii ya Wa-Taturu na viongozi wa mila walikazia Zaidi ridhaa yao kuhusiana na shughuli za EACOP na mchakato wa kushughulikia na kupunguza madhara mengine kama yatatokea kama ilivyo fafanuliwa kwenye Mpango wa EACOP na wasifu wa Jamii ya Mwamayoka. Hata hivyo, Jamii iliomba Bun'geda, kutokana na umihumi wa kipekee wa Ki-mila na Ki-ibada, Ziachwe. Hivyo basi, pande zote zilikubaliana kwa Pamoja kwamba bomba la mafuta lipindishwe kuepuka madhara (yatokanayo na uhamishwaji) kwa Bun'eda. Ramani inayo onesha upindishwaji huu kuepusha madhara kwenye Bung'eda ime ambatanishwa na kuitwa Kiambata 'A'.

Mengineyo kuhusiana na mchakato wa ushirikishwaji uliofanyika kwa kuzingatia mila na desturi na kuwezesha kufikiwa kwa makubaliano haya ya FPIC yame nakiliwa katika Muhutasari wa vikao na ripoti iliyo andaliwa na Mshauri wa EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni ZInazojitambua kama

Watu wa Asili, Dkt. Elifuraha Laltaika (Mtalam wa Kitanzania wa Haki za Jamii za Pembezoni). Nyaraka hiyo imeambatanishwa na Kiutwa Kiambata 'B'.

## Kusain Makubaliano ya FPIC

Imekubalika Kwamba Makubaliano ya FPIC yata sainiwa kwa wana Jamii wa Mwamayoka Tarehe 21 Machi 2023.

Siku ya Kusaini na uwezeshwaji wa EACOP yalikubaliwa kabla, katika kipindi cha ushirikishwaji wa wanajamii wa Ki-taturu na viongozi wao. Pamoja na wanajamii wa Ki-Taturu na viongozi wao, EACOP pia ime waalika wawakilishi wa Serikali ya Tanzania kushiriki katika utiaji sahihi.

## Majukumu ya Washauri na wawakilishi wa AZAKI.

Ili kuhakikisha makubaliano ya FPIC yameandaliwa kwa kuzingatia mila na desturi na kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa, ushirikishwaji wa ziada ulio wezesha kupatikana kwa Makubaliano haya ya FPIC yaliongozwa na Mshauri wa EACOP kwa Haki za Watu wa Pembezoni, Dkt. Elifuraha Laltaika, na kwa kupata maoni ya wana AZAKI wanao shiriki katika utekelezaji wa Mpango wa EACOP.

Zaidi ya hayo, katika kuthibitisha kwamba jamii imetoa ridhaa ya FPIC kwa kuzingatia kanuni za FPIC, wawakilishi wa AZAKI wanao wezesha utekelezaji wa Mpango wa EACOP watashiriki katika utiaji sahihi, na Dkt. Elifuraha Laltaika atashuhudia utiaji sahihi wa Makubaliano ya FPIC. Wata kagua nakala ya mwisho ya makubaliano ya FPIC na wana jamii na viongozi wa mila kabla ya kusainiwa ili kuhakikisha kwamba kuna uelewa mpana wa ridhaa ya Makubaliano.


## Uteuzi wa wawakilishi wa Jamii

Wawakilishi watatu wa Jamii watakao Saini Makubaliano ya FPIC kwa niaba ya wana jamii wa Mwamayoka wame teuliwa kwa uhuru na wana jamii kupita mchakato ambao umehusisha ushirikishwaji wa wana jamii, wanawake na vijana.

## Sahihi

Sisi ambao majina yetu yako hapa chini, tunatambua uwepo wa shughuli za EACOP kwa wakati huu na baadaye, na dhamira ya EACOP kushughulikia madhara makubwa na kuwezesha manufaa ya kiuchumi kwa wana jamii kwa mujibu wa Mpango wa EACOP, Wasifu wa Jamii ya Mwamayoka na Makubaliano haya ya FPIC kupindisha bomba la mafuta ili kuepusha madhara kwenye Bung'eda.

**Kiambata A**




*Kielelezo cha 1 – Ramani Inayo Onesha Kupindishiwa kwa Bomba la Mafuta la EACOP kukwepa Makaburi*

Makaburi yote yako eneo la KP 836+650 na 3 kati ya 4 karibu kabisa Katikati ya Mtaro wa bomba la mafuta – Chini ya mita 6

Mti wa 1: Tambiko hili lipo pembezoni wa ROW.

Mti wa 2: Tambiko liko mita 83 mbali na katikati ya mtaro wa bomba la mafuta na hauathiriwi

Kielelezo Cha 2: Mkakati unaotarajiwa kukwepesha madhara katika makaburi Mwamayoka.



**Kiambata B**

# MCHAKATO WA KUPATIKANA KWA RIDHAA HURU YA UELEWA (FPIC) NA JAMII YA WATATURU KITONGOJI CHA MWAMAYOKA, WILAYA YA IGUNGA:

# RIPOTI FUPI

## 1. Utangulizi

Ripoti hii ni muhutasari wa mchakato wa kupatikana kwa Ridhaa Huru ya Uelewa (FPIC) kwa Jamii ya Wa-Taturu wa Kitongoji cha Mwamayoka, Wilaya ya Iguga. Malengo ya Mchakato wa Makubaliano ya FPIC na ziara zilizofanywa yalikuwa kuwashirikisha wanajamii kwa mujibu wa mila na desturi, kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa shughuli za mradi wa bomba. Jamii imeridhia utekelezaji wa shughuli za EACOP katika ardhi yao, na haijaridhia uhamishwaji wa makaburi ambayo wameyaeleza kuwa yana umuhumu wa kipekee kimila na kimatambiko/kiibada.

## 2. Mchakato Wa Kupatikana Kwa Ridhaa Huru Ya Uelewa (FPIC) Na Jamii Ya Wataturu

Utafiti wa EACOP wenye kichwa cha Habari 'Utafiti wa Kijamii wa Jamii za Pembezoni wenye Uwezekano wa Kuathiriwana Mradi wa EACOP' (Utafiti wa Kijamii) unadhihirisha kwamba Wa-Taturu wana ukaribu mkubwa na ndugu zao waliotangulia mbele ya haki, hususan wazee maarufu. Huku ikitia mkazo Zaidi kwenye Utafiti wa Madhara ya Haki za Binadamu (HRIA), Tafiti za ESIA pamoja na RAP, Utafiti wa Kijamii ulithibitisha kwamba kwa Mwamayoka, Mradi wa EACOP unge athiri makaburi manne (yanaitwa Bung'eda kwa lugha ya Kitaturu), ya ukoo wa Masala. Baada ya hapo, EACOP iliwezesha ushirikishwaji kwa nyakati tofauti tofauti, kwa familia ya Masala na wana ukoo wengine.

Mzee Maarufu Mbushi Masala na Ali Masala (ambaye ni msemaji wa Ukoo) waliongoza majadiliano hayo. Katika mkutano uliofanyika Octoba 2021, familia ya Masala ilieleza kwamba wame shirikishwa vyakutosha kwa nyakati tofauti tofauti kuhusu uhamishwaji wa makaburi na kwamba wana ridhia yahamishwe.

Msemaji wa Ukoo alieleza kwamba malipo ya fidia yangehitajika ili kuwezesha wana familia kufanya ibada ya kuomba radhi mizimu ya wapendwa wao. Vile vile, gharama za kawaida za sherehe za Bung'eda zingehitajika. Sherehe hizo hufanyika anapofariki mzee

maarufu ambaye wazee wa rika lake wanamtambua kwamba ni maarufu na ana stahili sherehe ya aina hiyo.

Maamuzi yakisha fanyika, sherehe ambayo ina husisha uchinjaji wa ng'ombe dume, hufuata, na huweza kuendelea hadi kwa muda wa mwezi mmoja na nusu, kulingana na umaarufu wa mzee aliye tangulia mbele ya haki. Pamoja na kutanguliwa na huzuni, Bung'eda kwa kiasi kikubwa ni tukio la furaha ambalo huwaleta Pamoja mamia ya wana Kijiji kusherehekea Maisha ya mzee maarufu aliyetangulia mbele ya haki.

**3. Kubadilika kwa Uamuzi wa Wana-Jamii**

EACOP ili ridhia kwamba Jamii ya Wa-Taturu ilihitaji muda wa ziada kujadiliana wao kwa wao. Mwezi wa Nane 2022, Mshauri wa EACOP kwa Jamii za Pembezoni Zinazo Jitambua kama Watu wa Asili (Mshauri) alitembelea jamii ya Wa-Taturu kwa ajili ya ushirikishwaji Zaidi kuhusu uhamishwaji wa makaburi. Familia ya Masala na wana Ukoo kwa ujumla, waliemueleza Mshauri kwamba wamebadili maamuzi. Walieleza kwamba, kulingana na uelewa walio upata kutokana na kujengewa uwezo na kutokana na mikutano ya robo mwaka ya viongozi wa mila, Jamii wa Wa-Taturu imeamua kutoridhia kuhamishwa kwa makaburi, na Jamii inaiomba EACOP iheshimu uamuzi huo mpya.

Katika vikao kadhaa vilivyo huduriwa na wana Ukoo na majirani, wazee walipokezana kumuelimisha Mshauri wa EACOP kuhusu matambiko ya Bung'eda kwa jamii ya Wa-Taturu. Kwa mfano, wazee wali eleza kwamba miili huizikwi kwa kulaza kwenye makaburi, ila huzikwa kwa kukalishwa. Laana isiyotibika huwapata wahusika kama wakati wa mazishi, wanavunja mfupa wowote wa Marehemu.

Kuhusu makaburi ya sasa, wazee walieleza kwamba hakuna hata mmoja kati yao aliyewahi kushuhudia uhamishwaji wa makaburi, na kwamba walienda hadi Dirma (Kijiji kilichopo Wilaya ya Hanang) kutambika ila hawakupata 'ridhaa' kutoka kwenye mizimu, pamoja na kutumia gharama zao kufanya matambiko hayo. Wameelezea wasi wasi wao kwamba vifo vingi vinaweza kutokea endapo mizimu itakasirishwa kwa kuhamishwa.

**4. Maamuzi ya EACOP**

Kudhihirisha inavyo Heshimu Umuhimu wa mila na desturi pamoja na haki za binadamu za Jamii za Pembezoni zinazo jitambua kama Watu wa Asili, EACOP imethibitisha utayari wake kupindisha bomba la mafuta kuepusha madhara katika makaburi. Hili linadhihirisha nia njema

kwa upande wa EACOP lakini pia uimara wa ahadi zake za kuheshimu vigezo vya kimataifa kuhusu Jamii za Pembezoni zinazo jitambua kama watu wa Asili.

**5. Kusainiwa Kwa Mpango wa EACOP**

Uamuzi wa kupindisha bomba la mafuta ili kuepusha madhara ya kuhamishwa kwa Bun'geda ulifikiwa baada ya ushirikishwaji wa kina wa koo husika. Hivyo uamuzi ulifikiwa kwa Uhuru na kabla ya utelekezaji wa shughuli yeyote Mwamayoka. Mchakato huo uta hitimishwa na kunakiliwa kwa ku Saini Makubaliano ya FPIC kati ya Wa-Taturu na EACOP mbele ya Mshauri, Viongozi wa Serikali, na AZAKI zinazo saidia utekelezaji wa Mpango wa EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni zinazojitambua kama watu wa asili.

Imewasilishwa EACOP na:

Dkt. Elifuraha Laltaika (Mshauri wa EACOP-Jamii za Pembezoni zinazo jitambua kama watu wa Asili)

**Tarehe 09/03/2023**